

# NALIKULILIA UKANIPONYA.

PETER AMMI  
KIBOSHO SEMINARI  
28 Apr. 2022

Zab. Dom. 3 Pasaka Mwaka C

$\text{♩} = 58$

S  
A  
T  
B

Ee Bwa na Mu ngu wa ngu, na li ku li  
na li ku li li a Bwa na  
li a u ka ni po nya.

1. Ee Bwana nitakutukuza kwa maana umeniinua, wala hukuwafurahisha adui zangu juu yangu/  
Umeniinua nafsi yangu Ee Bwana kutoka kuzimu, umenihuisha,  
na kunitoa miongoni mwao washukao shimoni.
2. Mwimbieni Bwana zaburi enyi watawa wake, na kufanya shukrani kwa kumbukumbu la utakatifu wake/  
Maana ghadhabu zake ni za kitambo kidogo, katika radhi yake mna uhai, huenda kilio huja kukaa usiku,  
lakini asubuhi huwa furaha.
3. Ee Bwana usikie unirehemu, Bwana uwe msaidizi wangu, uligeuza matanga yangu kuwa machezo/  
Ulinivua gunia ukanivika furaha Ee Bwana Mungu wangu, nitakushukuru milele.